**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**

# MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA),

**MHESHIMIWA MHANDISI. HAMAD YUSSUF MASAUNI (MB),**

**AKIWASILISHA BUNGENI MAELEZO KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA UKUZAJI WA MAENDELEO YA KIJANI DUNIANI**

**(AGREEMENT ON THE ESTABLISHMENT OF THE GLOBAL GREEN GROWTH INSTITUTE)**

**Septemba, 2026** **DODOMA**

## MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA), MHESHIMIWA MHANDISI. HAMAD YUSSUF MASAUNI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAELEZO KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA UKUZAJI WA MAENDELEO YA KIJANI DUNIANI (AGREEMENT ON THE ESTABLISHMENT OF THE GLOBAL GREEN GROWTH INSTITUTE)

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninaomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute).

**Mheshimiwa Spika,** chimbuko la Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani ni Ibara ya 21 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani inayotoa nafasi kwa nchi kujiunga na Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Global Green Growth Institute (Taasisi ya GGGI)) baada ya kusainiwa kwa mkataba na kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo (Instrument of Accession) kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya GGGI ni taasisi ya kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya GGGI iliundwa rasmi tarehe 20 Juni 2012 ikiwa na nchi wanachama 5 baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI. Kwa mujibu wa Ibara ya 22, Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI ulianza kutekelezwa tarehe 18 Oktoba, 2012 baada ya nchi tatu (3) kuwasilisha Hati za Kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI. Hadi Mei 2026, Taasisi ya GGGI ilikuwa na wanachama 55 ambapo kati ya hao, 54 ni nchi wanachama na 1 ni Jumuiya ya Kikanda ambayo ni Organisation of Eastern Caribbean States (OECS). Aidha, nchi wanachama kumi na tatu (13) zinatoka Bara la Afrika ambazo ni Algeria, Angola, Benin,

Burkina Faso, Cote D'lvoire, Ethiopia, Morocco, Rwanda, Senegal, Togo, Uganda, Kenya na Zambia. Nchi za Afrika Mashariki ambazo zimejiunga na kufaidika na Taasisi hii ni Rwanda, Kenya na Uganda. Aidha, hadi kufikia Mei, 2026 nchi 28 zilikuwa zimeonesha nia ya kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa GGGI ambapo kati ya hizo nchi 16 zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Cameroon, Comoros, Djibouti, Gambia, Ghana, Misri, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Tunisia, São Tomé and Príncipe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tanzania na Zimbabwe. Aidha, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya pia uko katika mchakato wa kuwa mwanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya GGGI ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kusaidia taasisi za ndani za nchi wanachama kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani; kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi wanachama; kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wataalamu wa nchi wanachama katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

## 2.0 MADHUMUNI YA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA GGGI

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI ni kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani, kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi, kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani. Kigezo kimojawapo cha kunufaika na faida zitokanazo na Taasisi ya GGGI ni kuwa Mwanachama wa Taasisi hiyo.

## 3.0 IBARA ZA MKATABA NA MAUDHUI YAKE

**Mheshimiwa Spika**, mkataba huu una Ibara 28 naomba nielezee maudhui ya baadhi ya Ibara kwa ufupi kama ifuatavyo: -

**Ibara ya 2: Malengo Kuanzishwa kwa Taasisi ya GGGI**

Ibara hii inaeleza malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi ya GGGI ambayo ni kusaidia maendeleo endelevu kwa nchi wanachama hususan nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi (emerging economies) kwa: kusaidia na kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani; kuwezesha upatikanaji wa nafasi za ajira zenye staha; Kupunguza umasikini; kukuza ushirikishwaji wa jamii; kukuza hifadhi endelevu ya mazingira ikiwemo upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto na uhimilivu mabadiliko ya tabianchi; kukuza uhifadhi wa bionuai; na upatikanaji wa nishati safi na maji safi na salama kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea sekta ya umma na binafsi;

**Ibara ya 3: Tafsiri**

Ibara hii inatoa tafsiri ya mwanachama mchangiaji na mwanachama mshiriki. Mwanachama mchangiaji ni mwanachama ambaye anachangia kiasi kisichopungua dola za Marekani milioni 15 kwa kipindi cha miaka mitatu (3) au dola za Marekani milioni 10 kwa kipindi cha miaka miwili (2) ya kwanza ya uanachama wake na Mwanachama Mshiriki ni mwanachama wa GGGI ambaye siyo mwanachama mchangiaji;

**Ibara ya 4: Shughuli ya Taasisi ya GGGI**

Ibara hii inaelezea shughuli za Taasisi ya GGGI ambazo ni: Kusaidia nchi zinazoendelea kwa kuzijengea uwezo wa kubuni na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kwa kuzingatia dhana ya uchumi wa kijani; Kupunguza umasikini; Kuzalisha fursa za ajira na ushirikishwaji wa jamii; kufanya utafiti; Kuhamasisha ushirikiano kati ya Sekta za Umma na Binafsi ili kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ubunifu;

**Ibara ya 5: Uanachama**

Ibara hii inaeleza sifa za kuwa mwanachama wa Taasisi ya GGGI ambazo ni; nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa au kuwa Jumuiya ya Kikanda ambayo imekubali kutekeleza malengo ya taasisi kama yalivyoanishwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba;

**Ibara ya 12(1): Vyanzo vya Mapato**

Ibara hii inaeleza vyanzo vya mapato vya Taasisi ya GGGI ambavyo ni: - Michango ya hiari kutoka kwa wanachama wa Taasisi ya GGGI; Michango ya

hiari kutoka kwa Mashirika yasiyokuwa ya Serikali; Mauzo ya machapisho na mapato mengine; Riba kutokana na uwekezaji kwenye mifuko mbalimbali; na Mapato mengine kulingana na kanuni za fedha zilizoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taasisi ya GGGI;

**Ibara ya 15: Kinga na Upendeleo**

Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kutoa kinga na upendeleo kwa Taasisi ya GGGI ikiwemo mali na wafanyakazi wake kwa mujibu wa sheria;

**Ibara ya 21: Kuridhia Mkataba (Accession)**

Ibara hii inaeleza utaratibu wa nchi kujiunga na Taasisi ya GGGI baada ya kusainiwa kwa mkataba na kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo (Instrument of Accession) kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI;

**Ibara ya 22(2)** inaeleza utaratibu wa kuanza kuwa mwanachama kamili wa Taasisi ya GGGI ambapo nchi itakuwa mwanachama kamili siku ya 30 baada ya kuwasilisha Hati ya kuridhia kujiunga na Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI;

**Ibara ya 24: Marekebisho**

Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama ina haki ya kupendekeza marekebisho ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI kwa masuala ambayo yatakuwa na manufaa kwa nchi mwanachama;

**Ibara ya 25: Kujitoa Uanachama**

Ibara hii inaeleza kuhusu utaratibu wa kujitoa uanachama kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI ambapo utekelezaji wake utaanza rasmi (take effect) miezi sita (6) baada ya Mkurugenzi kupokea taarifa ya kujitoa; na

**Ibara ya 28: Kuvunjwa kwa Mkataba**

Ibara hii inaeleza utaratibu wa kuvunjwa kwa Mkataba ambapo hatua hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia maamuzi ya Mkutano Mkuu wa wanachama wote na utekelezaji wake utaanza mwaka mmoja (1) baada ya uamuzi kutolewa. Aidha, baada ya kuvunjwa kwa Mkataba wa GGGI, Taasisi ya GGGI itakoma.

## 4.0 MATOKEO NA FAIDA ZA KURIDHIA MKATABA WA GGGI

**Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI itaweza kunufaika katika masuala mbalimbali ikiwemo:

a) Kuongezeka kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

b) Kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

c) Kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani;

d) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi;

e) Kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

f) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa za ajira kwa watanzania;

g) Kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

h) Kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

## 5.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KURIDHIA MKATABA

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuridhiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, Serikali haitaweza kuweka maangalizo (reservations) kwa kuwa katika Ibara ya 23 ya Mkataba umezuia uwekwaji wa maangalizo (reservations) wakati wa kusaini au kuridhia Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute) kama ifuatavyo;

**KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa

Umoja wa Mataifa;

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mikataba hiyo inajumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC), Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (United Nations Convention to Combat Desertification - UNCCD) na Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai (Convention on Biological diversity - CBD);

**KWA KUWA**, Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani, kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi, kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

**KWA KUWA**, Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani ni taasisi ya kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto;

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadhamiria kujiunga kama Mwanachama mshiriki, itakuwa na wajibu wa kutoa kinga na haki za kidiplomasia kwa Taasisi ya Ukuzaji wa Kijani Duniani iwapo itajenga ofisi nchini;

**KWA KUWA**, madhumuni ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani yanajumusiha:-

(a) kusaidia na kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

(b) kuwezesha upatikanaji wa fursa za nafasi za ajira zenye staha;

(c) kupunguza umasikini;

(d) kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya hifadhi na

usimamizi wa mazingira na makabiliano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi;

(e) hifadhi endelevu ya mazingira ikiwemo upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto na uhimilivu mabadiliko ya tabianchi;

(f) kuwezesha uhifadhi wa bioanuai; na

(g) upatikanaji wa nishati safi na maji safi kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea sekta ya umma na binafsi.

**NA KWA KUWA**, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

(a) kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(b) kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(c) kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani;

(d) kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi;

(e) kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

(f) kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa ya ajira kwa watanzania;

(g) kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

(h) kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia Mkataba huo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Tatu, na kwa mujibu wa

masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako tukufu lijadili Azimio hili, na kuliridhia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhandisi Hamad M.Y. Masauni (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**